اليوم الآخر - سواحيلي

# HUKUMU
# ZA SIKU YA MWISHO


جمعية الدعوة بالزلفي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي

291

هاتف: ٠١٦ ٤٢٣٤٤٦٦ ـ فاكس: ٠١٦ ٤٢٣٤٤٧٧

# Hukumu za Siku ya Mwisho

## اليوم الآخر - سواحيلي

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات في الزلفي
هاتف: 164234466 966 ـ فاكس: 164234477 966

# Hukumu za Siku ya Mwisho

## أحكام اليوم الآخر

Katika misingi ya Imani na nguzo za Imani ni kuamini siku ya mwisho. Hawi mtu muumini wa kweli mpaka aamini yale yaliyokuja kwenye Kitabu cha Allah na yale yaliyokuwa sahihi katika Sunna za Mtume Rehema na Amani Zimfikie yanayo fungamana na siku hiyo.

Na kujua siku ya mwisho na kuikumbuka siku hiyo ni kitu muhimu sana. Kwani kuna athari kubwa katika kutengeza nafsi ya mwanadamu na kuitilia nguvu na kuisimamisha katika msimamo juu ya Dini ya Allah. Ili moyo usiwe na usususuwavu ukayaendea maasi, ukaghafilika na kuikumbuka siku ya mwisho na vituko vya siku hiyo na tabu zake. Ambazo Allah Amezisema katika Qur’an:-

﴿فَكَيْفَ تَتَّقُونَ إِنْ كَفَرْتُمْ يَوْمًا يَجْعَلُ الْوِلْدَانَ شِيبًا﴾ [المزمل:١٧]

*"Vipi mtakuwa wacha Mungu hali yakuwa mmeikanusha siku ambayo itamfanya mtoto kuwa mwenye mvi."* (Al-Muzamil: 17).

وقال تعالى: ﴿يَا أَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمْ إِنَّ زَلْزَلَةَ السَّاعَةِ شَيْءٌ عَظِيمٌ * يَوْمَ تَرَوْنَهَا تَذْهَلُ كُلُّ مُرْضِعَةٍ عَمَّا أَرْضَعَتْ وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ حَمْلٍ حَمْلَهَا وَتَرَى النَّاسَ سُكَارَى وَمَا هُمْ بِسُكَارَى وَلَكِنَّ عَذَابَ اللَّهِ شَدِيدٌ﴾ [الحج:١،٢]

*"Enyi watu mcheni Mola wenu hakika mtikisiko wa siku ya kiyama ni jambo kubwa sana, siku mtakayoona kila mwenye kunyonyesha anatelekeza kile anachokinyo-nyesha, na atazaa kila mwenye mimba kuizaa mimba yake, na utawaona watu kama vile wamelewa lakini sio walevi, lakini ni kutokana na adhabu kali ya Allah."* (Al-Haj: 1-2).

## Mauti

Mauti ndio mwisho wa kila kitu kilichopo hapa duniani. Allah Anasema:-

﴿كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ﴾ [آل عمران: ١٨٥]

*"Kila nafsi itayaonja mauti."* (Al-Imran: 185).

﴿ كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ﴾ [الرحمن:٢٦]

"*Kila kilichopo juu ya dunia ni chenye kuondoka.*" (Ar-Rahman: 26)

﴿ إِنَّكَ مَيِّتٌ وَإِنَّهُمْ مَيِّتُونَ ﴾ [الزمر:٣٠]

Allah Anasema kumwambia Mtume Wake:

"*Hakika yako wewe ni Maiti na hao pia ni maiti.*" (Az-Zumar: 30).

Hakuna yeyote atakayekaa milele katika hii dunia. Allah Anasema:-

﴿ وَمَا جَعَلْنَا لِبَشَرٍ مِنْ قَبْلِكَ الْخُلْدَ﴾ [الأنبياء:٣٤]

"*Na Hatukumfanya mwanadamu kabla yako kuishi milele.*" (Al-Anbiyaa: 34).

Na katika aya hii kunaashiria mambo yafuatayo;

1. Hakika watu wengi wameghafilika na mauti, pamoja na kuwa mauti ni jambo la lazima ambalo halina shaka kabisa. Basi ni juu ya kila Muislamu kufanya wingi wa kuyakumbuka mauti na kujiandaa kwa ajili ya mauti. Na kubeba zawadi kutoka duniani kwa ajili ya akhera kwa kufanya matendo mema kabla ya kuondoka hapa duniani.

قال الرسول ﷺ: ((اغتنم خمسًا قبل خمس، حياتك قبل موتك، وصحتك قبل سقمك، وفراغك قبل شغلك، وشبابك قبل هرمك، وغناك قبل فقرك )) [رواه الإمام أحمد]

Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema: *"Faidika na mambo matano kabla hayajakufika mambo matano, uhai wako kabla hayajakufika mauti yako, afya yako kabla ya ugonjwa wako, faragha yako kabla ya shughuli yako, ujana wako kabla ya uzee wako na utajiri wako kabla ya ufakiri wako."* (Ameipokea Imam Ahmad).

Elewa na kutambua ya kuwa mauti hayabebwi pamoja na vitu vyako kwenda navyo kaburini. Kwani kitakachobakia pamoja nawe ni matendo yako. Fanya pupa katika kufanya matendo mema ambayo yatakufanya upate mazuri mbele ya Allah na upate ufaulu wa milele na ili uweze kufaulu kwa kuepuka kutokana na adhabu kwa Uwezo Wake Allah.

2. Ajali ya mwanadamu imejificha haijulikani. Hakuna yeyote anayeijua isipokuwa ni Allah Pekee. Kwani hakuna mtu mwenye kujua lini atakufa au sehemu gani atakufa. Na hii ndio `*ilimul -ghaib* ambayo Allah Anaistahili Yeye Pekee.

3. Mwanadamu akijiwa na mauti hawezi kuyazuia au kuyacheleweshа au kuyakimbia. Allah Anasema:

﴿وَلِكُلِّ أُمَّةٍ أَجَلٌ فَإِذَا جَاءَ أَجَلُهُمْ لا يَسْتَأْخِرُونَ سَاعَةً وَلا يَسْتَقْدِمُونَ﴾ [الأعراف:٣٤]

*"Kila umma unao ajali yake, ikifikia ajali yao haitakawia nao japokuwa kwa muda mfupi wala hawatautangulia."* (Al-A'raf: 34).

4. Muumini akijiwa na mauti, anajiwa na Malaika mwenye sura nzuri, mwenye harufu nzuri, wanahudhuria pamoja naye Malaika wazuri wakimbashiria pepo. Allah Anasema;

﴿إِنَّ الَّذِينَ قَالُوا رَبُّنَا اللهُ ثُمَّ اسْتَقَامُوا تَتَنَزَّلُ عَلَيْهِمُ الْمَلائِكَةُ أَلَّا تَخَافُوا وَلا تَحْزَنُوا وَأَبْشِرُوا بِالْجَنَّةِ الَّتِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ﴾ [فصلت:٣٠]

*"Hakika wale ambao wanasema Mola wetu ni Allah, kisha wakalingana sawa (wakawa na msimamo) watateremkiwa na Malaika, wakiwaambia msikhofu wala msihuzunike, kuweni na bishara njema ya kuipata pepo ambayo mlikuwa mmeahidiwa."* (Fuswilat: 30).

Na ama kafiri atajiwa na Malaika wa mauti kwa sura ya kutisha, uso mweusi, watakuja na pamoja naye Malaika wa adhabu wakimbashiria kupata adhabu. Mwenye Mungu Anasema:

﴿وَلَوْ تَرَى إِذِ الظَّالِمُونَ فِي غَمَرَاتِ الْمَوْتِ وَالْمَلائِكَةُ بَاسِطُو أَيْدِيهِمْ أَخْرِجُوا أَنْفُسَكُمُ الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ عَذَابَ الْهُونِ بِمَا كُنْتُمْ تَقُولُونَ عَلَى اللهِ غَيْرَ الْحَقِّ وَكُنْتُمْ عَنْ آيَاتِهِ تَسْتَكْبِرُونَ﴾ [الأنعام:٩٣]

*"Na lau wawaona madhalimu nao wapo kwenye vitisho vya mauti, ungaliona jambo la kufazaisha, huku Malaika wakizitwaa roho zao, wameikunjua mikono yao kwa adhabu, watawaambia zitoeni nafsi zenu, leo mtadhalilishwa upeo wa kudhalilishwa, kama mlivyokuwa mkisema uongo juu ya Allah na mkiona kiburi kufuata Aya Zake na kuandama Mitume Wake."* (A'anam: 93)

Pindi mauti yakija kunadhihirika kila jambo la mwanadamu. Allah Anasema:

﴿حَتَّى إِذَا جَاءَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ رَبِّ ارْجِعُونِ لَعَلِّي أَعْمَلُ صَالِحاً فِيمَا تَرَكْتُ كَلَّا إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَائِلُهَا وَمِنْ وَرَائِهِمْ بَرْزَخٌ إِلَى يَوْمِ يُبْعَثُونَ﴾ [المؤمنون: ٩٩، ١٠٠]

*"Mpaka yamjie mmoja wao mauti atasema nirudisheni duniani nikafanye matendo mema katika yale niliyoyaacha, sivyo hivyo hakika hilo ni neno limeshasemwa na nyuma yake kuna kizuizi mpaka siku ya kufufuliwa."* (Muuminuna: 99 – 100).

Pindi mauti yakija atatamani kafiri na mwenye kufanya maaswi kurudi duniani ili aje afanye matendo mema, lakini majuto hayatamfaa chochote baada ya kupitwa na wakati. Allah Anasema:

﴿وَتَرَى الظَّالِمِينَ لَمَّا رَأَوُا الْعَذَابَ يَقُولُونَ هَلْ إِلَى مَرَدٍّ مِنْ سَبِيلٍ﴾

**[الشورى:٤٤]**

*"Na utawaona madhalimu siku ya kiyama watakapoiona adhabu, wakisema kumwambia mola wao, je kuna njia yoyote ya kurejea duniani ili tufanye matendo ya utiifu kwako?"* (As-Shura: 44)

5. Kutokana na Rehma kwa waja Wake kwamba ambae atakuwa mwisho wa maneno yake ni kusema: ***Laailaaha Illallah***, ataingia peponi, amesema Mtume Rehema na Amani Zimfikie:

قال ﷺ: ((من كان آخر كلامه من الدنيا، لا إله إلا الله دخل الجنة))

**[أخرجه أبو داود]**

*"Yeyote atakayekuwa mwisho wa maneno yake kutoka duniani ni* ***Laailaaha Illallah*** *ataingia peponi."* (Ameipokea Abu Daud)

Kwani haiwezi kuisema mwanadamu wakati huo mzito isipokuwa mwenye Ikhlasi kwenye hilo neon. Ama yule ambaye hakuwa na ikhlasi kwenye hilo neno hataweza kulitamka kutokana na shida iliyompata ya uchungu wa mauti. Ni sunna kwa wale watakaokuwa wapo kwa mtu anayekaribia kufa wamlakinie hili neno la ***Laailaaha Illallah*** kila mara. Kutokana na kauli yake Mtume Rehema na Amani Zimfikie aliposema:

لقول النبي ﷺ: ((لقنوا موتاكم لا إله إلا الله))[رواه مسلم:٩١٦]

*"Walakinieni wanaokaribia kifo neno la Laailaaha Illallah."* (Muslim: 916).

Sio kwa kumlazimisha asije akapaniki akatamka maneno yasiyokuwa ya sawa.

***Talkini***: Ni kulirudia rudia neno na yule anayekusikia analitamka kwa kukufatilizia.

## Kaburi

Imepokewa na Anas Allah Amuie Radhi anasema; Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema: *"Hakika mja anapowekwa kwenye kaburi lake na watu wake wakaondoka, hakika yake anasikia vishindo vya viatu vyao."*

Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema: *"Mtu akiwekwa kaburini anajiwa na malaika wawili watamkalisha, watamuambia: 'Ulikuwa ukisemaje kuhusu huyu mtu?' Mtume akasema: 'ikiwa ni muumini atasema: 'Nashuhudia ya kwamba ni mja wa Allah na Mtume Wake.' Akasema Mtume: 'Ataambiwa: Angalia makazi yako motoni, hakika Allah Amekubadilishia makazi yako katika pepo.' Mtume wa Allah akasema: 'Ataona vyote viwili pepo na moto.' Ama Kafiri au Mnafiki atasema atakapoulizwa: 'Sijui, kwani nilikuwa nikisema kama walivyokuwa wakisema watu.' Ataambiwa, 'wala hautajua wala kuelewa.' Kisha atapigwa kwa nyundo ya chuma pigo moja kati ya masikio yake mawili, atapiga kelele atasikia yule aliye karibu naye isipokuwa viumbe viwili; majini na watu."* (Bukhari na Muslim)

Kurudi kwa roho kwenye kiwiliwili ni katika mambo ya akhera ambayo akili ya kibinadamu haiwezi kufikiria katika dunia. Hakika waislamu wote

wanakubaliana yakuwa mwanadamu anapata neema mbali mbali kaburini. Akiwa ni muumini mwenye kustahiki neema, au ataadhibiwa ikiwa anastahiki adhabu, ikiwa hajachupa mipaka ya Allah. Allah Anasema:

﴿النَّارُ يُعْرَضُونَ عَلَيْهَا غُدُوًّا وَعَشِيًّا وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ أَدْخِلُوا آلَ فِرْعَوْنَ أَشَدَّ الْعَذَابِ﴾ [غافر:٤٦]

*"Kwanza walipatikana na gharika wakaanga-mia kisha wakawa wanaadhibiwa ndani ya makaburi yao ambapo moto unadhi-hirishwa kwao asubuhi na jioni, mpaka wakati wa kuhesabiwa, na siku ambayo kiyama kita simama kutasemwa: Watieni motoni jamaa wa Firaun katika adhabu kali."* (Ghafir: 46).

قال الرسول ﷺ: ((تعوذوا بالله من عذاب القبر)) [رواه مسلم:٢٨٦٧]

Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema: *"Jilindeni kwa Allah kutokana na adhabu ya kaburi."* (Muslim: 2867).

Akili iliyosalimika haiwezi kupinga hayo kwani mwanadamu katika maisha yake anayaona yaliyo karibu na hayo. Mwenye kulala anahisi ni kwamba anaadhibiwa adhabu kali, atapiga kelele na kuomba

msaada lakini wa pembezoni mwake asihisi chochote. Kuna tofauti kubwa kati ya mauti na uhai, na adhabu katika kaburi na roho pamoja na kiwiliwili.

قال الرسول ﷺ: ((إن القبر أول منزل من منازل الآخرة، فإن نجا منه فما بعده أيسر منه، وإن لم ينج منه فما بعده أشد منه))

**[أخرجه الترمذي:٢٢٣٠]**

Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema: *"Hakika ya kaburi ni kituo cha kwanza katika vituo vya Akhera, akifaulu mtu katika kituo hicho basi vyote vitakavyokuja baada yake vitakuwa vyepesi. Ikiwa hatafaulu katika kituo hicho basi vyote vitakuwa ni vigumu kwake kuvipita."* (Ameipokea Tirmidhiy: 223)

Inatakikana kwa Muislamu kufanya wingi wa kujikinga na adhabu ya kaburi hasa hasa kabla ya kutoa salamu kutoka kwenye Swala. Na awe na pupa ya kujiepusha na kufanya maasi ambayo ni sababu ya mwanzo ya mtu kuadhibiwa katika kaburi na kuingizwa motoni. Kwa hakika imeitwa adhabu ya kaburi kwa sababu watu wengi watafunikwa ndani yake. Isipokuwa yule ambae amegharikika kwenye maji au ameungua na moto au ameliwa na wanyama wakali na mfano wake. Mtu huyo hataadhibiwa au atapata neema katika maisha ya barzakhi.

Adhabu za kaburini zipo za aina mbali mbali. Ipo ya kupigwa kwa nyundo ya chuma na vitu vinginevyo. Kiza kutanda ndani ya kaburi. Kutandikiwa ndani ya kaburi moto na kufunguliwa mlango wa motoni. Na kufananishiwa matendo yake na mtu mwenye uso mbaya wenye harufu mbaya, atakaa pamoja naye kwenye kaburi lake, na adhabu itaendelea ikiwa mtu ni kafiri au mnafiki. Ama ikiwa mja mwema lakini ni mwenye kufanya madhambi, adhabu yake itatofautiana kulingana na maasi yake, inaweza ikakatika adhabu kwake.

Ikiwa mtu ni muumini atapata neema mbali mbali katika kaburi lake na kupanuliwa. Kaburi lake ndani yake litajaa nuru. Atafunguliwa mlango miongoni mwa milango ya peponi na itamjia harufu nzuri na atatandikiwa vitu vya peponi. Na matendo yake yatafananishwa katika sura ya mtu mwema mzuri atakayekuwa akimliwaza katika kaburi lake.

## Kisimamo cha Kiyama na Alama Zake.

1. Allah Hakuumba huu ulimwengu ili ubakie milele, isipokuwa utajiwa na siku ambayo itakuwa ni yenye kuumaliza. Na siku hii ndio kitasimama kiyama, ambayo ni haki hakuna shaka ujio wa siku hiyo.

﴿إِنَّ السَّاعَةَ لَآتِيَةٌ لا رَيْبَ فِيهَا وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لا يُؤْمِنُونَ﴾

[غافر:٥٩]

*"Hakika ya kiyama ni chenye kuja hakina shaka ndani yake lakini watu wengi hawaamini."* (Ghafir: 59)

﴿وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لا تَأْتِينَا السَّاعَةُ قُلْ بَلَى وَرَبِّي لَتَأْتِيَنَّكُمْ﴾

**[سبأ:٣]**

*"Wakasema wale ambao wamekufuru hakitatujia kiyama, sema: Ninaapa kwa Mola wangu kwa hakika kitawajia…"* (Sabaa: 3).

﴿اقْتَرَبَتِ السَّاعَةُ﴾ **[القمر: ١]**

*"Kwa hakika kimekaribia kiyama."* al-Qamar:1

﴿ اقْتَرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ وَهُمْ فِي غَفْلَةٍ مُعْرِضُونَ﴾ **[الانبياء:١]**

*"Hakika imekaribia watu kuhesabiwa juu ya matendo yao na hali yakuwa wapo kwenye hali ya kupumbaa na kuipa nyongo onyo hili."* (Al-Anbiyah: 1).

Lakini kukaribia kwake sio kwa makisio ya mwanadamu na kufahamu kwa mwanadamu

isipokuwa ni kulingana na Allah Anavyojua katika yale yaliyopita katika dunia.

Na kukijua kiyama ni katika *Ilmul Ghaibi* ambayo Anaijua Allah Peke Yake. Hajamfundisha wala Kumuelekeza kiumbe yeyote katika viumbe Wake. Allah Anasema:

﴿يَسْأَلُكَ النَّاسُ عَنِ السَّاعَةِ قُلْ إِنَّمَا عِلْمُهَا عِنْدَ اللهِ وَمَا يُدْرِيكَ لَعَلَّ السَّاعَةَ تَكُونُ قَرِيبًا ﴾[الأحزاب:٦٣]

*"Wanakuuliza watu kuhusiana na kiyama, waambie: Ilimu yake ipo kwa Allah, na lipi lililo kujulisha wewe, uenda kiyama kikawa ni karibu kutokea."* (Al-Ahzab: 63).

Bwana Mtume Rehema na Amani Zimfikie alizitaja alama zinazojulisha kukaribia kwa kutokea kiyama miongoni mwazo ni;

Kutokea kwa Masihi Dajjal ambaye ni fitna kubwa kwa watu. Allah Amemkadiria katika kufanya mambo ya kutengeneza yasiyokuwa ya kweli na watadanga-nyika watu wengi kutokana na mambo yake. Ataiamrisha mvua inyeshe itanyesha. Ataamrisha majani kuota yataota. Atafufua maiti na mengi mengineyo katika mambo ya kutengeneza. Bwana

Mtume Rehema na Amani Zimfikie alimtaja Masihi Dajjal akasema kuwa ni mtu mwenye chongo, katika moja ya macho yake. Na atakuja na mfano wa pepo na moto, kile ambacho atasema kuwa ni pepo, basi huo ndio moto na ule anaosema ndio moto basi hiyo ndio pepo. Atakaa hapa duniani kwa muda wa miaka arobaini. Siku moja ni kama mwaka mmoja, siku moja kama mwezi, siku moja kama wiki, kisha siku zinazobakia ni kama siku za kawaida. Hakuna sehemu yoyote katika ardhi hii isipokuwa ataingia isipokuwa ardhi ya Makka na Madina tu.

Kushuka kwa Issa *Alayhi Ssalam*, Mwana wa Mariamu, atashukia juu ya mnara mweupe upande wa mashariki mwa mji wa Damascus (Syria). Wakati wa Swala ya asubuhi, ataswali pamoja na watu Swala ya asubuhi kisha atamtafuta Dajjal na kumuua.

Katika alama za kiyama ni kuchomoza kwa jua kutokea magharibi. Watu watafadhaika na kuamini wakati ambapo haitawafaa chochote kuamini kwao. Na kuna alama nyingi za kiyama.

2. Hakitasimama kiyama isipokuwa kwa watu waovu. Allah Atatuma kabla ya kusimama kwake upepo mzuri utakaozichukua roho za waumini. Atakapotaka Allah Kuwamaliza viumbe Wake ni kuwaletea kifo na

kuiondoa dunia kwa kumtuma Malaika apulize parapanda (Pembe kubwa), wakiisikia wanaadamu watakufa wote. Allah Anasema:

﴿وَنُفِخَ فِي الصُّورِ فَصَعِقَ مَنْ فِي السَّمَاوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ إِلَّا مَنْ شَاءَ اللَّهُ﴾ [الزمر:٦٨]

*"Na itapulizwa parapanda na watakufa wote waliopo mbinguni na ardhini isipokuwa wale Anaowataka Allah wasife."* (Az-Zumar: 68)

Na tukio hilo litatokea siku ya Ijumaa. Kisha baada ya hapo watakufa malaika wote, hakutabaki kiumbe wa aina yeyote isipokuwa atabakia Mwenyewe Allah Peke Yake.

3. Kila mwili wa mwanadamu utaisha na utaliwa na ardhi isipokuwa kifupa cha ncha ya mgongo kitabakia. Lakini miili ya Mitume na mashahidi haitaliwa na ardhi. Allah Atateremsha maji kutoka mbinguni kuja kuotesha mili na kuiunganisha upya.

Allah Atakapotaka Atawahuisha watu kwa kumuhuisha Malaika Israfil ambaye ni Malaika wa kupuliza parapanda. Atapuliza parapanda kwa mara ya pili na watafufuka viumbe wote kutoka makaburini

mwao. Na watakuwa kama Alivyowa-umba Allah mara ya kwanza, wakiwa peku peku wako uchi, wenye magovi. Allah Anasema:

﴿وَنُفِخَ فِي الصُّورِ فَإِذَا هُمْ مِنَ الْأَجْدَاثِ إِلَى رَبِّهِمْ يَنْسِلُونَ﴾ [يٓس:٥١]

*"Na kutapulizwa parapanda mpulizo wa pili, hapo roho zirudishwe kwenye miili yao, wakitahamaki wanatoka makaburini mwao wakielekea kwa Mola wao kwa haraka."* (Yasin: 51)

﴿يَوْمَ يَخْرُجُونَ مِنَ الْأَجْدَاثِ سِرَاعًا كَأَنَّهُمْ إِلَى نُصُبٍ يُوفِضُونَ * خَاشِعَةً أَبْصَارُهُمْ تَرْهَقُهُمْ ذِلَّةٌ ذَلِكَ الْيَوْمُ الَّذِي كَانُوا يُوعَدُونَ﴾

[المعارج:٤٣، ٤٤]

*"Siku watakapotoka makaburini wakienda kwa haraka, kama walivyokuwa duniani wakienda mbio na haraka kwa waungu wao wakiwaabudu badala ya Allah, hali ya kuwa macho yao ni madhalilifu yanatazama chini, wamefunikwa na unyonge na utwevu, hiyo ndiyo siku waliyoahidiwa duniani."* (Al-Ma'arij: 43 – 44).

Mtu wa mwanzo ambaye ardhi itapasuka ili atoke ni Mtume wa mwisho; Mtume Muhammad Rehema na Amani Zimfikie kama ilivyokuja kwenye hadithi. Kisha

watu wataswagwa kwenda kwenye ardhi ya kukusanywa watu (Ardhi ya *Mahshari*). Nayo ni ardhi pana sana iliyotandikwa vizuri isiyokuwa na bonde. Na watakusanywa makafiri kwa nyuso zao. Aliulizwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie, 'namna gani watakusanywa makafiri kwa nyuso zao?' Akajibu Mtume Rehema na Amani Zimfikie kama alivyosema kwenye hadithi yake;

وقد سئل الرسول ﷺ: كيف يُحشر الكافر على وجهه؟ فقال: ((أليس الذي أمشاه على رجليه في الدنيا، قادرًا على أن يمشيه على وجهه يوم القيامة)). [رواه مسلم: ٢٨٠٦]

Aliulizwa Mtume Rehema na Amani Zimfikie, 'namna gani atakavyokusanywa kafiri katika uwanja wa kukusanywa watu?' Mtume akajibu akasema: *"Sio yule ambaye alikuwa akitembea kwa miguu miwili duniani, akiwa na uwezo wa kutembelea, atatembelea juu ya uso wake siku ya Kiyama."* (Ameipokea Muslim: 2806).

Mwenye kukataa utajo wa Allah na kuipinga Qur'an atafufuliwa siku ya kiyama akiwa kipofu. Na siku hiyo jua litasogea karibu na viumbe na kila kiumbe atatoka jasho kutokana na matendo yake aliyoyafanya hapa duniani. Wapo miongoni mwao watakaotoka jasho na kufikia kwenye vifupa viwili

vya miguuni na wako ambao jasho litatoka na kujaa mpaka kwenye kiuno, na wako ambao litawafika mpaka shingoni kadiri ya matendo yao. Na wako ambao Allah Atawafunika kwa Kivuli Chake siku ambayo hakuna kivuli isipokuwa Kivuli Chake.

قال الرسول ﷺ: ((سبعة يظلهم الله ـ تعالى ـ في ظله يوم لا ظل إلا ظله: الإمام العادل، وشابٌ نشأ في عبادة الله، ورجلٌ قلبه معلقٌ في المساجد، ورجلان تحابا في الله، اجتمعا عليه وتفرقا عليه، ورجلٌ دعته امرأةٌ ذات منصب وجمال فقال: إني أخاف الله، ورجلٌ تصدق بصدقة فأخفاها حتى لا تعلم شماله ما تنفق يمينه، ورجلٌ ذَكَرَ الله خاليـًا ففاضت عيناه) [متفق عليه: ١٤٢٣-١٠٣١]

"Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema: *"Watu wa aina saba Allah Atawafunika katika Kivuli Chake siku ambayo hakuna kivuli isipokuwa Kivuli Chake: Imamu muadilifu, kijana aliyekulia katika ibada ya kumuabudu Allah, mtu ambaye moyo wake umefungamana na misikiti, watu wawili waliopenda na kwa ajili ya Allah na wakakutana kwa ajili Yake na wakatengana kwa ajili ya Allah, mtu ambaye aliyeitwa na mwanamke mwenye nafasi na cheo na uzuri ili afanye naye uchafu lakini akamjibu: 'Mimi ninamuogopa Allah', mtu ambaye alitoa sadaka kwa kificho, haukujua mkono wa kushoto kilichotolewa na*

*mkono wa kulia, na mtu ambaye amemtaja Allah Peke Yake mpaka macho yake yakatokwa na machozi."* (Ameipokea Bukhari na Muslim: 1424 – 1031)

Siku hiyo kiu kitakuwa kikali kwa watu. Siku ambayo inakadiriwa kama miaka elfu hamsini, lakini atapita muumini kwa haraka kama vile kutekeleza Swala ya faradhi. Na waislamu watakunywa katika birika la Mtume Rehema na Amani Zimfikie (Birika tukufu kubwa). Watakunywa humo umma wake siku ya kiyama. Maji yake ni meupe zaidi kuliko maziwa na ni matamu kuliko asali. Na harufu yake ni nzuri zaidi kuliko harufu ya miski. Na vyombo vyake vya kutumia ni vingi kama idadi ya nyota mbinguni. Mwenye kunywa kutoka kwenye hilo birika funda moja tu hatopata kiu baada yake kabisa.

Watabakia watu katika ardhi ya kukusanywa kwa muda mrefu wakisubiria kutenganishwa kati yao na kuhesabiwa. Wakiwa wamesimama muda mrefu na kusubiri pamoja na kuwa kuna shida kubwa ya joto kali la jua. Watamtafuta ambae atawaombea kwa Allah ili wahukumiwe kati ya viumbe. Watamuendea Nabii Adam *Alayhi Ssalam*, naye atatoa udhuru. Kisha watamuendea Nabii Nuhu *Alayhi Ssalam,* naye atatoa udhuru. Kisha watamuendea Nabii Ibrahim *Alayhi*

*Ssalam*, naye atatoa udhuru. Kisha watamuendea Nabii Mussa *Alayhi Ssalam,* naye atatoa udhuru. Kisha watamuendea Nabii Issa *Alayhi Ssalam,* naye atatoa udhuru. Kisha watamuendea Nabii Muhammad Rehema na Amani Zimfikie, atasema, *'mimi ndio mwenye ummah huu',* baada ya hapo atasujudu chini ya A'rshi ya Allah na atamuhimidi Allah haki ya kumuhimidi. Allah Atamfungulia sehemu aliyopo Mtume kwa kumuambia:

((يا محمد! ارفع رأسك، وسل تعط، واشفع تشفَّع))

*"Ewe Muhammad nyanyua kichwa chako, omba utapewa, omba msamaha utasamehe-wa."*

Allah Atatoa idhini ya kuhukumiwa na kuhesabiwa, na ummah Muhammad ndio utakaokuwa wa kwanza kuhesabiwa.

Jambo la mwanzo kuhesabiwa katika matendo yake mja aliyoyatenda ni Swala. Ikiwa Swala yake itakuwa ni yenye kutengemaa vizuri na kukubalika basi ataangaliwa katika matendo mengine. Na ikiwa Swala yake itarudishwa basi matendo yake yote yatarudishwa.

(يُسأل العبدُ عن خمس: عن عمره فيم أفناه، وعن شبابه فيم أبلاه، وعن ماله من أين اكتسبه وفيم أنفقه، وعن علمه ماذا عمل به).

"*Ataulizwa mja siku ya kiyama kuhusiana na mambo matano: Kuhusu umri wake ameumalizaje? na kuhusu ujana wake ameutumia vipi? na kuhusu mali zake amezichumaje na amezitoaje? na kuhusu elimu yake ameifanyia kazi gani?*" Ama jambo la mwanzo kuhukukumiwa kati ya waja ni kuhusu kulipiza kisasi cha kumwaga damu.

Na kisasi siku hiyo ni kupeana mema na mabaya, yatachukuliwa mema ya mtu na kupewa yule hasimu yake, na yakiwa mema yake yameisha yatachukuliwa mabaya ya hasimu yake na kurushiwa juu yake.

Na itasimamishwa *Swirata* (Na hiyo *Swirata* ni daraja jembamba kuliko nywele, na ni kali kuliko upanga, na itasimamishwa katika kuta za Jahannam). Na watapita watu juu yake kwa kiasi cha uzwingi na uzito wa matendo yake, wako miongoni mwao watakaopita kwa haraka kama kufumba na kufumbua. Wengine kama upepo, wengine kama mwendo wa farasi na wako wengine watatambaa

kwa mikono. Na kwenye *Swirata* kuna kingoe atakao wachukua makafiri na kuwatupa motoni. Na wataanguka makafiri na wengine Anaowataka Allah katika waliofanya maasi katika waumini na wataingia motoni. Lakini makafiri watakaa motoni milele. Na kuhusu waliofanya maasi wataadhibiwa Atakapo Allah kisha watatolewa motoni na kuingizwa peponi.

Allah Atampa Idhini Amtakaye katika Mitume na Manabii na miongoni mwa waja wema kuwaombea baadhi ya waliongia motoni katika watu wa *Tawheed* na Allah Atawatoa motoni. Na atasimama mwenye kupita kwenye *Swirata* (nao ni watu wa peponi) juu ya daraja lililopo kati ya motoni na peponi kwa kulipiziwa kisasi baadhi yao kwa wengine.

Hataingia peponi yule ambaye ana vitu vya dhulma alivyomdhulumu ndugu yake mpaka alipiziwe ili nafsi za wengine zitulie vizuri. Watakapoingia watu wa peponi - peponi na wakaingia watu wa motoni - motoni, mauti yatakuja kwa sura ya kondoo atakayechinjwa kati ya motoni na peponi. Watu wa motoni na peponi wataangalia kisha kutasemwa: "Enyi watu wa peponi kaeni milele peponi hakuna kifo. Enyi watu wa motoni kaeni milele motoni hakuna kifo."

Na laiti kama mtu anaweza kufa kwa furaha basi angekufa kwa furaha mtu wa peponi kutokana na kufurahi zaidi. Na laiti mtu angeweza kufa kwa huzuni basi angekufa mtu wa motoni.

## Moto na Adhabu Zake.

قال تعالى: ﴿ فَاتَّقُوا النَّارَ الَّتِي وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ أُعِدَّتْ لِلْكَافِرِينَ ﴾ [البقرة:٢٤]

*"Uogopeni moto ambao kuni zake ni watu na mawe, moto ambao umeandaliwa makafiri kuingia humo."* (Al-Baqarah: 24)

وقال رسول الله ـ ﷺ ـ لأصحابه: ((ناركم هذه ـ التي يوقد ابن آدم ـ جزء من سبعين جزءا من حرِّ جهنم)) قالوا: والله إن كانت لكافية، يا رسول الله، قال: ((فإنها فضلت بتسعة وستين جزءًا، كُلها مثل حرِّها)) [رواه البخاري ومسلم: ٣٢٦٥، ٢٨٤٣]

Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema kuwaambia Maswahaba zake: *"Moto wenu huu – (ambao mwanadamu anauwasha) – ni fungu miongoni mwa mafungu sabini ya moto wa Jahanam.' Wakasema Maswahaba: 'Ewe Mtume wa Allah, Wallah unaweza kuwa ni wenye kutosha.' Mtume*

*akasema: "Kwa hakika umefadhwilishwa kwa mafungu sitini na tisa yote yanafanana joto lake."* (Ameipokea Bukhari na Muslim: 3265, 2843)

Moto una tabaka saba, kila tabaka moja ina adhabu

kali kushinda nyingine na kila tabaka ina watu wake watakaoingia kadiri ya matendo yao. Na wanafiki watakuwa chini kabisa katika moto. Nayo ni adhabu kali kushinda zote. Na adhabu ya watu wa motoni ambao ni makafiri itakuwa ni ya kudumu sio yenye kukatika. Na kila watakapoungua wanarudishwa tena mara nyingine ili waongezewe adhabu. Allah Anasema:

﴿كُلَّمَا نَضِجَتْ جُلُودُهُمْ بَدَّلْنَاهُمْ جُلُودًا غَيْرَهَا لِيَذُوقُوا الْعَذَابَ﴾ [النساء:٥٦]

*"Kila zinapoiva na kuungua ngozi zao Tunazibadilisha ngozi nyingine, ili wapate kuionja adhabu."* (An-Nisaa: 56)

﴿ وَالَّذِينَ كَفَرُوا لَهُمْ نَارُ جَهَنَّمَ لا يُقْضَى عَلَيْهِمْ فَيَمُوتُوا وَلا يُخَفَّفُ عَنْهُمْ مِنْ عَذَابِهَا كَذَلِكَ نَجْزِي كُلَّ كَفُورٍ﴾ [فاطر:٣٦]

*"Na wale ambao wamemkufuru Allah, watakuwa na moto wa Jahanam uliowashwa, hakutatolewa uamuzi*

*juu yao kuwa wafe wakapata kufa na kupumzika wala hawatapunguziwa adhabu yake, mfano wa malipo hayo Tunamlipa kila mwenye kuendelea kufanya ukafiri."* (Fatir: 36)

Makafiri watafungwa ndani ya moto shingo zao. Allah Anasema:

﴿وَتَرَى الْمُجْرِمِينَ يَوْمَئِذٍ مُقَرَّنِينَ فِي الْأَصْفَادِ * سَرَابِيلُهُمْ مِنْ قَطِرَانٍ وَتَغْشَى وُجُوهَهُمُ النَّارُ﴾ [ابراهيم:٤٩-٥٠]

*"Na utawaona Ewe Nabii waasi siku ya kiyama wamefungwa pingu mikono yao na miguu yao imekutanishwa na minyororo na hali ya kuwa ni wanyonge. Nguo zao ni za rojo la mafuta linalochemka sana, na hapo moto utaziramba nyuso zao na kuzichoma."* (Ibrahim: 49-50)

Chakula cha watu wa motoni ni *Zaquum*. Allah Anasema:

﴿إِنَّ شَجَرَتَ الزَّقُّومِ * طَعَامُ الْأَثِيمِ * كَالْمُهْلِ يَغْلِي فِي الْبُطُونِ * كَغَلْيِ الْحَمِيمِ﴾ [الدخان:٤٣-٤٨]

*"Hakika mti wa zaquum unatoka kwenye shina la moto wa Jahim, ni chakula cha mtu mwenye dhambi nyingi, ni kama madini yaliyoyeyu -shwa yanayochoma kwenye matumbo. Kama vile maji yanayochemka yaliyofikia upeo wa joto."* (Ad-Dukhan: 43-46)

Allah Anabainisha adhabu kali ya moto siku ya kiyama na neema kubwa ya pepo siku ya kiyama, kama ilivyokuja kwenye Sahihi Muslim;

في صحيح مسلم عن النبي ﷺ، أنه قال: ((يؤتى بأنعم أهل الدنيا، من أهل النار، يوم القيامة، فيصبغ في النار صبغة، ثم يقال: يا ابن آدم، هل رأيت خيرًا قط؟ هل مرَّ بك نعيمٌ قط؟ فيقول: لا، والله يا رب، ويؤتى بأشدِّ الناس بؤسًا في الدنيا، من أهل الجنة، فيصبغ صبغة في الجنة، فيقال له: يا ابن آدم، هل رأيت بؤسًا قطُّ؟ هل مر بك شدةٌ قط؟ فيقول: لا، والله يا رب، ما مر بي بؤس قطُّ، ولا رأيت شدةً قطُّ)) [رواه مسلم: ٢٨٠٧]

Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema: *"Zitaletwa neema mbali mbali za watu wa duniani kwa watu wa motoni siku ya kiyama zitawekwa kwenye moto na kuacha athari yake kwa uzuri wake, kisha ataulizwa: 'Ewe mwanadamu, je haujawahi kuona kheri yoyote*

*kushinda hii? Je haijawahi kukupitia neema nzuri kushinda hii?' Atasema: 'Hapana sijawahi ewe Mola wangu Mlezi.' Ataletewa mtu masikini duniani katika watu wa peponi, na utawekwa umasikini wake ndani ya pepo, kisha ataambiwa: 'Ewe mwanadamu je, alishawahi kuona umasikini zaidi ya huu? Na je, ulishawahi kukupitia umasikini zaidi ya huu?' Atasema: 'Hapana ewe Mola wangu Mlezi, haujawahi kunipitia umasikini kabisa na wala sijawahi kuona shida kabisa."* (Ameipokea Muslim: 2807).

Kafiri atasahau kila kitu kilichopita kwake duniani kutokana na neema mbali mbali kwa kuzamishwa mara moja ndani ya moto. Na Muumini atasahau kila kilicho msusuaza katika mambo ya dunia katika ufakiri na ubaya kwa kuzamishwa katika pepo.

## Namna ya Pepo Ilivyo.

Pepo ni nyumba ya kudumu na ni nyumba tukufu, Allah Amewaandalia waja Wake wema. Ndani yake kuna neema mbali mbali ambazo hakuna jicho lililowahi kuziona, wala hakuna sikio lililowahi kuzisikia, wala hakuna hata chembe katika moyo wa mwanadamu kumpitia na kuzifikiri. Allah Anasema:

﴿فَلا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَا أُخْفِيَ لَهُمْ مِنْ قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ﴾ [السجدة:١٧]

*"Nafsi ya mwanadamu haijui katika yale yaliyofichika katika pumbazo la macho yake, hayo ni malipo kwa yale waliyokuwa wakiyafanya duniani."* (As-Sajidah: 17)

Kuna daraja mbali mbali, tofauti tofauti, kwa waumini peponi watakazofikia kutokana na ukubwa wa matendo yao. Allah Anasema:

﴿يَرْفَعِ اللهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَالَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ دَرَجَاتٍ﴾

[المجادلة:١١]

*"Allah Anawanyanyua vyeo miongoni mwenu na Anavipandisha vyeo vya wenye elimu daraja nyingi."* (Al-Mujadilah: 11).

Waumini watakula na kunywa ndani ya pepo kile kinachotamaniwa na nafsi zao. Ndani ya pepo kuna mito ya maji yasiyoharibika. Na kuna mito ya maziwa yasiyobadilika ladha yake (yasiyochacha), freshi kabisa. Kuna mito ya asali safi. Na kuna mito ya pombe yenye ladha nzuri kwa wenye kuinywa. Pombe yao sio kama pombe ya duniani. Allah Anasema:

﴿يُطَافُ عَلَيْهِمْ بِكَأْسٍ مِنْ مَعِينٍ ۞ بَيْضَاءَ لَذَّةٍ لِلشَّارِبِينَ ۞ لا فِيهَا غَوْلٌ وَلا هُمْ عَنْهَا يُنْزَفُونَ﴾ [الصافات:٤٥-٤٧]

*"Zinazungushwa kwao glasi za pombe inayotoka kwenye mito inayotembea, hawa chelei kuwa itamalizika. Ni nyeupe rangi yake, ni tamu katika kuinywa. Haina madhara yoyote ya akili wala ya mwili."* (As-Swafaat: 45-47).

Na wataozeshwa ndani ya pepo wanawake (*Mahurule'n*). Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema:

((لو أن امرأة من أهل الجنة أطلعت إلى أهل الأرض لأضاءت ما بينهما – أي السماء والأرض – ولملأته ريحا)) [رواه البخاري:٢٧٩٦]

*"Laiti mwanamke mmoja wa peponi ajitokeze kwa watu wa ardhini wamuone basi ungeenea mwanga kati ya mbingu na ardhi na kungejaa harufu nzuri."* (Ameipokea Bukhari: 2796)

Na neema kubwa wakayoipata watu wa peponi ni kumuona Allah Mtukufu. Watu wa peponi hawataenda haja ndogo wala haja kubwa, wala hawatapenga kamasi wala hawatatema mate kwa harufu mbaya. Vichanio vyao ni vya dhahabu na

watarashiwa mafuta ya miski. Neema yao hii ni ya milele, haitakatika kabisa wala haitapungua. Mtume Rehema na Amani Zimfikie anasema:

قال ﷺ: ((من يدخل الجنة يَنْعم لا يبأس، لا تبلى ثيابه، ولا يفتى شبابه)) [رواه مسلم: ٢٨٣٦]

*"Mwenye kuingia peponi ameneemeka hana shaka kabisa, nguo zake hazitachakaa ujana wake hautaondoka."* (Ameipokea Muslim: 2836).

Kiasi kidogo watakachopewa watu wa peponi - naye ni yule atakayetolewa motoni katika watu wa Imani na ataingia peponi - ni mazuri yote ya duniani mara kumi.